

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA
UPIMAJI WA KITAIFA WA DARASA LA NNE

03

MAARIFA YA JAMII

Muda: Saa 1:30

MAJIBU

Mwaka: 2023

Maelekezo

1. Karatasi hii ina sehemu A na B zenye jumla ya maswali manne (4).
2. Jibu maswali yote katika kila sehemu.

maktaba.tetea.org



SEHEMU A (ALAMA 26)

Jibu maswali yote katika sehemu hii.

1. Jibu kipengele (i) – (viii) kwa kuchagua herufi ya jibu sahihi kisha andika katika kisanduku uliyopewa.

(i) Yapi ni mazao ya biashara yanayolimwa Tanzania?

- A. Mahindi, chai na kahawa
- B. Pamba, chai na kahawa
- C. Ndizi, kahawa na pamba
- D. Mihugo, mpunga na tumbaku

B. Pamba, chai na kahawa

Haya ni mazao ya biashara kwa sababu hulimwa kwa ajili ya kuuzwa ndani na nje ya nchi na kuingizia taifa mapato.

(ii) Ipi ni faida ya utalii nchini Tanzania?

- A. Kuiga mila na desturi za wageni
- B. Kupata fedha za kigeni
- C. Kuongezeka kwa mazao ya misitu
- D. Kuongezeka kwa wanyama pori

B. Kupata fedha za kigeni

Utalii huingizia nchi fedha za kigeni kupitia wageni wanaotembelea vivutio vya utalii.

(iii) Madini ya almasi yana matumizi gani?

- A. Kukatia vioo
- B. Chanzo cha nishati ya joto
- C. Kukatia chuma
- D. Kuzalisha umeme

A. Kukatia vioo

Almasi ni ngumu sana hivyo hutumika kukatia vioo na vifaa vigumu.

(iv) Mbuga ipi ni kubwa kuliko yote nchini Tanzania?

- A. Ruaha
- B. Ngorongoro
- C. Mikumi
- D. Serengeti

A. Ruaha

Mbuga ya Ruaha ndiyo kubwa zaidi nchini Tanzania kwa ukubwa wa eneo.

(v) Bainisha wanyama wanaofugwa kati ya wafuatao:

- A. Simba, ng'ombe na kondoo
- B. Pundamilia, kondoo na chui
- C. Twiga, kondoo na mbuzi
- D. Mbwa, kondoo na mbuzi

D. Mbwa, kondoo na mbuzi

Hawa ni wanyama wa kufugwa nyumbani tofauti na wengine ambao ni wanyama pori.

(vi) Ipi ni njia sahihi ya kutunza misitu?

- A. Kuchoma miti ili kupunguza msongamano
- B. Kuzalisha mkaa ili kuongeza kipato
- C. Kupanda miti mingine baada ya kukata ya awali
- D. Kujenga maeneo ya misitu ili kupata hewa safi

C. Kupanda miti mingine baada ya kukata ya awali

Njia hii husaidia kurejesha uoto wa asili na kulinda misitu isiishe.

(vii) Ni madini yapi hutumika kutengeneza saruji?

- A. Chuma
- B. Chokaa
- C. Fosfeti
- D. Chumvi

B. Chokaa

Chokaa ni malighafi muhimu inayotumika katika utengenezaji wa saruji.

(viii) Kwanini kilimo ni uti wa mgongo kwa uchumi wa Tanzania?

- A. Huvutia watalii wengi
- B. Watu wengi wameajiriwa kwenye kilimo
- C. Watu wengi huishi mashambani
- D. Wawekezaji wengi wamewekeza kwenye kilimo

B. Watu wengi wameajiriwa kwenye kilimo

Kilimo huajiri idadi kubwa ya Watanzania na kuwa chanzo kikuu cha kipato.

2. Jibu kipengele cha (i) – (vi) kwa kuoanisha mchango wa mashujaa wa Tanzania katika Fungu A na majina yao katika Fungu B. Andika herufi ya jibu sahihi kwenye mabano uliyopewa.

(i) Aliwaongoza Waafrika kupinga uvamizi wa Wajerumani katika eneo la Kilwa Kivinje 1890

C. Abushiri Bin Sultan

(ii) Alianzisha sera ya soko huria

F. Ali H. Mwinyi

(iii) Aliwaongoza Wazigua kupinga uvamizi wa Wajerumani katika eneo la Tanga mwaka 1890

E. Bwana Heri

(iv) Alitekeleza sera ya elimu bure kwa wote kuanzia darasa la awali hadi kidato cha nne

B. John P. Magufuli

(v) Aliwaongoza Wayao wa Masasi na Tunduru kupigana na Wajerumani mwaka 1890

A. Chief Mchemba

(vi) Alianzisha mfumo wa ubinafsishaji

D. Benjamin W. Mkapa

3. Soma kifungu cha habari kifuatacho kisha jibu maswali yanayofuata kwa kuandika jibu sahihi katika nafasi iliyoachwa wazi.

(a) Kwanini ni muhimu kuishi katika mazingira safi?

Ni muhimu kuishi katika mazingira safi kwa sababu **hupunguza kuenea kwa magonjwa na hulinda afya ya binadamu.**

(b) Ni kiumbe hai kipi ambacho kina sumu ambacho huweza kudhuru watu na viumbe wengine?

Kiumbe huyo ni **nyoka.**

(c) Kwa kuzingatia kifungu cha habari, taja kifaa kimoja kinachotumika kufanya usafi. Kifaa kimoja ni **jembe.**

(d) Ni ugonjwa gani unaweza kuepukwa kwa kufyeka nyasi na kuondoa maji yaliyotuama?

Ugonjwa unaweza kuepukwa ni **malaria.**

(e) Ni mdudu yupi anaweza kusababisha kuenea kwa ugonjwa wa kipindupindu?

Mdudu huyo ni **inzi.**

(f) Kutokana na habari uliyosoma, wadudu na wanyama hatarishi hupatikana wapi?

Hupatikana **katika mazingira machafu kama majani marefu na maji yaliyotuama.**

(g) Ni namna gani tunaweza kuwa na mazingira safi?

Tunaweza kuwa na mazingira safi kwa kufanya usafi kila siku, kufyeka nyasi na kufukia mashimo yenye maji.

4. Chora alama za ramani kuonesha vitu vifuatavyo.

(a) Mlima – alama ya pembetatu

(b) Daraja – mstari wenye mapengo juu ya mto

(c) Reli – mistari miwili sambamba yenye vijiti katikati

(d) Kiwanja cha ndege – alama ya ndege